BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Tisa – Tarehe 19 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa

mwaka 2021/2022.

II. **MASWALI:**

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

150. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Uzoefu unaonesha kwamba, katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba endapo wafanyakazi wa Serikali watapata uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba hutakiwa kukaa huko kwa kipindi cha miaka miwili na baadae kurudi Unguja. Lakini wapo wafanyakazi wengi ambao wameshafanyakazi Pemba kwa muda mrefu bila ya kurudishwa Unguja

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea hali hii.

(b) Je, hatuoni kwamba kuwaweka wafanyakazi hawa kwa muda mrefu ni kuwapunguzia morali ya kufanya kazi.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

127. MHESHIMIWA ZAINA ABDALLA SALUM (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza sana Serikali yangu kwa kuamua kuweka utaratibu mzuri wa fedha za wajasiriamali wetu wa makundi maalum. Fedha ambazo zilikuwa zikitolewa na Halmashauri za Manispaa zetu lakini sasa zimewekewa utaratibu wa kuziingiza katika Mfuko wa Uwezeshaji, hivyo kuyafanya maombi ya fedha za makundi hayo yafanyike kwenye Mfuko wa Uwezeshaji.

(a) Kwakuwa fedha hizo zilikuwa ni kwa ajili ya makundi maalum kupitia Halmashauri za Manispaa, Je, mpaka hivi sasa ni kiasi gani cha fedha kilichoingizwa.

(b) Kwakuwa fedha hizi zinachanganywa na fedha za Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Je, kuna utaratibu gani unaotumika ili kuwanufaisha walengwa waliokusudiwa.

(c) Kwakuwa Halmashauri na Manispaa zetu zinatenga fedha kupitia makusanyo yao na kuziingiza katika Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa lengo la kuwasaidia vikundi vidogo vidogo kwa makundi maalum, Je, kuna mgongano au changamoto gani katika utowaji wa fedha hizo.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

26. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na changamoto ya uchakavu na ufinyu wa nafasi katika ofisi zote za Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya zake zote tatu, hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwa watumishi wa Ofisi hizi.

(a) Kwa kuwa muda mrefu kumekuwa na wazo la kuzijenga Ofisi hizo Je, ni lini ujenzi huo utaanza.

(b) Ni lini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ilifanyiwa ukarabati na iligharimu kiasi gani cha fedha.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

99. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusiana na tofauti iliyopo kati ya bei halisi ya uingizaji bidhaa nchini na bei ambayo wafanyabiashara hulazimishwa kuiandika kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi ya VAT. Aidha, kumekuwa na uingizwaji wa kodi ya ziada ya VAT ndani ya nchi kwa bidhaa kama mchele, unga wa ngano, sukari na mafuta ya kupikia, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu na makubaliano ya kodi na tozo za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na malalamiko hayo.

(b) Je, ni zipi asilimia na ni utaratibu upi sahihi wa kutoza kodi ya VAT kwa bidhaa hizo tokea zinapotoka nje hadi kumfikia mlaji.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

137. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, iliahidi kukisaidia kikundi cha Nguvu Hazichezewi cha Mvumoni - Jimbo la Wawi

kinachojishughulisha na masuala ya ufugaji wa samaki na kuvuna chumvi.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kukisaidia kikundi hicho ili kizidi kupiga hatua.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

101. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na maagizo ya Serikali kuhusiana na ufungaji wa mita za umeme na upatikanaji wa nguzo za umeme kwa wananchi wanaohitaji kuungiwa huduma ya umeme Unguja na Pemba, kumekuwa na malalamiko ya kuwepo utapeli unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi halali wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) na baadhi ya waajiriwa wa Wizara yako bila ya kuchukuliwa hatua stahiki.

(a) Je, ni hatua gani Serikali inawachukulia wafanyakazi wanaothibitika kuwatapeli wananchi katika kuungiwa umeme.

(b) Je, Serikali inawalipa fidia gani wananchi hao, baada ya kuthibitika kuwa wametapeliwa na wafanyakazi wa taasisi zake.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

118. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa mnamo mwezi wa Novemba 2022 dunia inatarajiwa kushuhudia mashindano makubwa ya mpira wa miguu ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini Qatar. Na kwa kuwa kwa miaka mingi tumeshuhudia Vyombo vya Habari vya Serikali TVZ sasa ZBC vikionyesha moja kwa moja kupitia televisheni, mashindano mbali mbali ya mpira wa miguu duniani.

(a) Je, Shirika la ZBC¬-TV limejindaa vipi kuonesha moja kwa moja (live) mashindano hayo kwa wananchi wote wa Zanzibar.

(b) Je, Shirika la ZBC-TV limeshatayarisha mpango wowote wa biashara za matangazo kupitia mashindano hayo.

(c) Je, kuna wadhamini wa aina gani waliojitokeza mpaka

hivi sasa kudhamini matangazo ya kombe la dunia kupitia ZBC-TV/Redio.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

144. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Huduma za wananchi zimeondolewa kutoka Kituo cha Afya cha zamani kilichopo shehia ya Banda Kuu Nungwi na kupelekwa maeneo ya kijiji cha maafa kilichopo kilomita mbili na nusu kutoka kijiji cha Nungwi.

(a) Je, ni lini kituo hicho cha zamani kitafanyiwa matengenezo ili huduma irudi hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wanashindwa kwenda masafa marefu kuifuata huduma ya afya.

(b) kwa kuwa ndani ya kituo hicho cha zamani panatolewa huduma nyengine mbali na zile za afya. Je, ni nani hao wanaotoa huduma na ni huduma gani wanayoitoa.

(c) Je, Wizara yako iko tayari kufika kijijini Nungwi na ikutane na wananchi, ili kusikia mahitaji yao hasa katika kituo cha zamani mlichohamisha huduma za afya.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

15. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kijiji cha kibokoni Kisiwani Pemba, kilimo cha karanga kinaonekana kushamiri zaidi na kuwaletea tija wakulima wa kilimo hiki.

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia elimu wananchi wa Kibokoni juu ya kilimo cha karanga kwa lengo la kuwawezesha kulima kilimo chenye tija.

(b) Ni lini Wizara ya Kilimo itawapatia mashine za kukamulia karanga wananchi hao ili waweze kuzalisha mafuta.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

43. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa ujenzi wa madarasa na skuli tofauti Unguja na Pemba. Pamoja na juhudi kubwa za ujenzi huo, skuli zetu nyingi zina uhaba mkubwa wa vitendea kazi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzipatia vitendea kazi skuli zetu zikiwemo skuli ya Kiembesamaki msingi A na B, Kiembesamaki sekondari A na B.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**19 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**